(١)

Katika Makaribisho ya Safari ya Israa na Miraji.

Prof.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mtukufu, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu:

{SUBHANA, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuoneshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona).

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana mshirika wake na ninashuhudia kuwa Bwana wetu Muhammad ni Mja na Mtume wake. Ewe Mola wetu msalie na ummbariki yeye na Jamaa zake na Maswahaba wake na kila atakaye ufuata mwongozo wake kwa wema mpaka siku ya Malipo.

Na baada ya utangulizi huu,
Katika jambo ambalo halina shaka ni kwamba Safari ya Mtume S.A.W ya Israa na Miraji ina siri nyingi kubwa; kwani ni safari ya aina yake katika Historia ya Binadamu. Safari hii ilikuja kwa lengo la kumkirimu Mtume S.A.W, Mwisho wa Manabii na Mitume, na kwa kumpa Mtume S.A.W furaha baada ya miaka ambayo alionja yeye na Maswahaba wake aina mbali mbali za ukandamizwaji na kufanyiwa maudhi pamoja na kukadhibishwa, na baada ya kupomteza  ami yake Abuu Twaalib kwa muda wa siku kadhaa ndani ya mwaka wa kumi tangu apewe Utume, ambaye alikuwa ndio tegemeo lake kubwa katika maisha yake, na kufiwa na mkewe Bi Khadija R.A, mwenye

busara nyingi, mpole, ambaye alikuwa ngome na kimbilio lake lenye usalama alilolikimbilia wakati wa shida.
Ari ya Mtume S.A.W iliongezeka baada ya safari ya Twaaif yenye majonzi ambayo ilikuwa ni katika mazingira magumu mno katika maisha yake Mtukufu huyu wa Daraja. Na baada ya kuumizwa na maudhi ya Watu wake na Watu wengine, Mtume S.A.W alitoka na kuelekea Twaaif akiwa na matumaini huwenda akapata unafuu au nusura, lakini wao wakawa na maudhi zaidi na roho ngumu mno, kwani wao walimuadhibu wote, watumwa na watoto wao wakawa wanamrushia mawe mpaka damu ikawa inamtoka miguuni mwake Mtukufu huyu wa Daraja. Na akaamua S.A.W kuelekea katika njia ya kurejea kwa Mola Wake Mtukufu kwa dua hii yenye upendo ndani yake ambayo inabeba kila aina ya maana za Uja na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, yeye tu na wala sio kwa mwingine, akasema: Ewe Mola wangu, kwako wewe ninakulalamikia unyonge wa nguvu zangu, na uchache wa hila zangu na udhaifu wangu kwa Watu, ewe Mwingi wa wenye Rehema wenye. Wewe ni Mola wa wanyonge. Na wewe ni Mola wangu, unaniacha na nani niendako? Nielekeako (ugenini) wanakonishambulia? kwenye ugumu zaidi? Au adui uliyemmilikisha Jambo langu? Kama wewe hujanikasirikia mimi sichukulii lakini msamaha wako kwangu ni mpana zaidi, ninajikinga kwako kwa nuru ya uso wako ulioangaza viza na Jambo la Dunia na akhera likatengemaa, usiniteremshie hasira ghadhabu zako au hasira zako zikanikuta, wewe ni mwenye kunyenyekewa mpaka uridhie, na hakuna ujanja au nguvu isipokuwa kutoka kwako.

Na kuanzia hapa, na katika kitovu cha mitihani yote hii, Mtihani mkubwa wa kiungu ni safari ya Israa na Miraji ambayo mwenyezi Mungu Mtukufu alimwonesha mja wake Mtume Muhammad S.A.W, uhalisia wa mambo yasiyoonekana na siri mbali mbali za Ulimwengu huu ambazo hakuna mfalme yoyote aliye karibu alna Mwenyezi Mungu Mtukufu, au nabii yoyote aliyetumwa, aliwahi kuyaona hayo

isipokuwa Mtume Muhammad S.A.W kama ni heshima kubwa kwake na kumtia nguvu moyoni mwake ili imani, yakini na kujiamini viongezeke na kujua kwamba yeye yuko katika msaada wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na katika malezi yake na ulinzi wake pia.

Hakika Muujiza wa Israa na Miraji ni katika miujiza mitukufu na ni alama kubwa miongoni mwa alama ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mkweli aliyetukuka alimkirimu Mtume wake Muhammad S.A.W. Na sisi katika kukaribisha tukio hili la kukumbukwa, na tusimame katika baadhi ya masomo na mazingatio yenye manufaa kwetu yatokanayo na Tukio hili.

Hakika Muujiza wa Israa na Miraji haukinzani na ukweli wa kumtegemea mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwani yeye alimdhalilishia Mtume wake Muhammad S.A.W mnyama Buraq awe kipando chake safarini pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuwa na uwezo wa kumsafirisha usiku bila ya kutumia njia yoyote iwayo, na ingawa Mtume S.A.W alikuwa na yakini kamili na imani yake ya kumtegemea mwenyezi Mungu Mtukufu, isipokuwa alipowasili katika Msikiti wa Aqswaa alimfunga mnyama Buraq aliyedhalilishwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama ni funzo kwa Umma wake kwamba kuna umuhimu wa kuchukua nyenzo kazi katika kila jambo, akasema S.A.W: Nikamfunga kwa fundo litumiwalo na Mitume. Anasema Imamu Nawawiy: Na katika kumfunga Buraq kuna uchukuaji wa tahadhari katika mambo, na kutumia nyenzo. Na kwamba Jambo hili halipotezi maana ya kumtegemea mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwani Muumini wa kweli hufanya kazi ambayo haimuokoi isipokuwa kazi yake hiyo na kumtegemea mwenyezi Mungu Mtukufu kwa utegemeaji ambao anajua fika kuwa hakuna chochote kitakachompata isipokuwa alichomwandikia Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na uelewa huu uwianifu ndilo kusudio la kauli ya Mtume S.A.W aliposema Kuhusu utumiaji wa nyenzo: Kama mmoja wenu kitamkuta Kiama na katika mkono wake ana mche wa kupandwa basi na aupande.

Ba katika kauli yake Mtume S.A.W kwa upande wa kumtegemea mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: Kama nyinyi mnategemea Mwenyezi Mungu Mtukufu ukweli wa kumtegemea angekuruzukuni kama anavyowaruzuku ndege, wao hutoka wakiwa na matumbo matupu na hurejea wakiwa wameshiba.
Ndugu wa Manabii na Mitume wote, Mitume wote ni wabeba ujumbe mmoja katika Chimbuko na Akida zote, hata kama watatofautiana katika Sheria na Mfumo. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu}.

{وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ}

Na anasema Mtume wetu S.A.W: Mitume ni Ndugu kwa miunganiko ya Mama zao mbali mbali na Dini yao Moja.

Bwana wetu Abdullah bin Abas. R.A anasema kuhusu nyasia kumi ،

zilizokuja katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema: {Sema: Njooni nikusomeeni aliyo kuharimishieni Mola wenu Mlezi. Nayo ni kuwa, msimshirikishe Yeye na chochote. Na wazazi wenu wafanyieni wema. Wala msiwauwe watoto wenu kwa sababu ya umasikini. Sisi tunakuruzukuni nyinyi na wao. Wala msikaribie mambo machafu, yanayo onekana, na yanayo fichikana. Wala msiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameharimisha kuiuwa, ila ikiwa kwa haki. Hayo amekuusieni ili myatie akilini

Wala msiyakaribie mali ya yatima ila kwa njia ya wema kabisa, mpaka afikilie utu-uzima. Na timizeni vipimo na mizani kwa uadilifu. Sisi hatumkalifishi mtu ila kwa kadiri ya uwezo wake. Na msemapo semeni kwa uadilifu ingawa ni jamaa. Na ahadi ya Mwenyezi Mungu itekelezeni. Hayo amekuusieni ili mpate kukumbuka. Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia

nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kumcha Mungu}.

**Hizi ni aya ni za Hukumu ambazo hazijafutwa katika Sheria yoyote miongoni mwa Sheria au Dini katika Dini. Nazo ni mambo yaliyoharamishwa kwa wanadamu wote. Na ni Msingi na uti wa mgongo wa sheria. Na yoyote atakayezifanyia kazi ataingia Peponi, na atakayeziacha ataingia Motoni.**

Na katika alama kubwa ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu alimkirimu Mtume waje S.A.W ilikuwa ni kuwakusanya Mitume wote na Manabii katika Msikiti wa Baitul Maqdis, na Mtume S.A.W akawaswalisha kama Imamu wao, kama ambavyo walimpokea Mtume S.A.W katika umbingu wa juu wakisema: Karibu Mtume Mwema na Ndugu Mwema. Na hiyo ilikuwa idhini ya kuuhamisha uimamu wa ardhini na kumkabidhi Mtume S.A.W, na wakati huo huo kutekeleza kivitendo makubaliano na ahadi aliyoichukua Mwenyezi Mungu Mtukufu juu yao ambapo anasema:

{Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hikima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha mliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mmekiri na mmekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia}

Wakasema, Ali bin Abuu Twaalib na Abdullahi bin Abas R.A: Mwenyezi Mungu Mtukufu hajawahi kumtuma Mtume yoyote katika Mitume isipokuwa alichukua ahadi juu yake iwapo atampa Utume Muhammad na Mtume huyo mwenye ahadi akawa yuko hai basi atamwamini Muhammad na atamnusuru, na akamwamrisha aichukue ahadi hiyo juu ya Umma wake, iwapo atampa Utume

Muhammad S.A.W na Mitume hao wakiwa hai basi wote watamwamini yeye na kumnusuru.

Nafasi ya Msikiti wa Aqswaa pamoja na Msikiti wa Makkah:

Mtume S.A.W aliishia katika msikiti huo wa Aqswaa katika Israa kisha akaanzia hapo safari ya Miraji kuelekea mbingu za juu kisha katika Sidratil Muntahaa. Msikiti huo pia ni kibla cha kwanza kabla ya Kibla cha pili, na ni wa tatu kati ya Misikiti mitatu mitakatifu ambayo inatembelewa kwa wingi kwa ajili ya swala na thawabu zake. Kama ambavyo huu ni msikiti wa pili kujengwa Duniani. Na kutoka kwa Abuu Dharri R.A amesema: alisema: nilisema, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Ni Msikiti upi uliojengwa kwanza Duniani? Mtume Akasema: Msikiti wa Makkah. Mimi nikasema: kisha msikiti upi? Akasema: kisha Msikiti wa Aqswaa. Nikasema: ni umbali upi uliokuwepo kati ya misikiti hii miwili? Akasema: Ni miaka arubaini kisha popote itakapokukuta swala basi swali kwani ndani yake kuna fadhila nyingi. Na Swala ndani yake ni bora kuliko Swala khamsini katika misikiti mingine isipokuwa Msikiti wa Makkah na Msikiti wa Madina ambapo Mtume S.A.W anasema: Fadhila za Swala katika Msikiti wa Makkah kwa misikiti mingine ni sawa na Swala elfu moja, na fadhila za swala katika Msikiti wa Madina ni sawa na Swala elfu moja, na fadhila za swala katika Msikiti wa Aqswaa ni sawa na Swala mia tano.

Kwa hiyo Msikiti wa Aqswaa ni sehemu isiyogawika ya vitakatifu vya Uislamu. Kwa hiyo Msikiti huu una nafasi kubwa katika nyoyo za Umma wa Muhammad S.A.W. Nao ni amana katika dhima ya Waislamu wote na haipaswi kuiachia au kuizembea katika kuilinda. Kama ambavyo ni wajibu wetu kupandikiza maana hii kwa watoto wetu mpaka vizazi vijavyo visije vikasahau nafasi na utakatifu wa Msikiti wa Aqswaa kwa Waislamu wote.

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

* * *

**Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na rehma na amani ziwe juu ya wa Mwisho katika Mitume, na Wajumbe wake, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote.**

Ndugu zangu Waislamu.

Kwa kuanza kwa mwezi wa nne kila Mwaka, Ulimwengu mzima huadhimisha siku ya Mtoto Yatima, na kwamba mafunzo ya Dini yetu samehevu ya Uislamu, yamezitangulia taasisi zote za kibinadamu katika kumlea mtoto yatima na kumtimizia haki zake. Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:
{Na wanakuuliza juu ya mayatima. Sema: Kuwatengenezea ndio kheri. Na mkichanganyika nao basi ni ndugu zenu; na Mwenyezi Mungu anamjua mharibifu na mtengenezaji. Na Mwenyezi Mungu angeli penda angeli kutieni katika udhia. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima}.

Na mzingativu yoyote wa aya hii ya Quran tukufu anaona kwamba maelezo ya Qurani yamekuja kwa neno "kuwatengenezea" ili likuwe kusanyifu la kila aina ya matunzo na malezi. Kwani kutengeneza ni jina kusanyifu la kila kinachohitajika. Kunaweza kuhitajika mali, na utengenezaji ukawa ni wema na utoaji wa mali, na huwenda Mtoto Yatima akawa tajiri na kwa hivyo akahitaji unyooshwajicna malezi, na

hivyo, utengenezaji hapo ukawa ni matunzo na malezi. Na Mtoto Yatima anaweza kuwa anahitaji Mtu wa kumfanyia biashara zake kwa mali aliyonayo au anaeweza kumsaidia shughuli za kilimo au kiiwandani kwake na haoo utengenezaji unakuwa kwa kuyafanya hayo. Na anaweza kuwa hahitaji hiki wala kile isipokuwa anahitaji upole na upendo na kupata hisia za uzazi na ukawa huo ndio utengenezaji wenyewe kwa kumtekelezea hayo. Na inawezekana kabisa kumnyoosha pale alipokengeuka au alipopinda kimaadili na kumfundisha mwenendo na tabia yake zikawa njema. Na kwa maana hiyo kusanyifu ya malezi na matunzo, zimekuja aya za Quran tukufu na Hadithi za Mtume S.A.W zikituasa na kutulingania tuzitengeneze hali zote za Yatima na kuyachunga mambo yake yote.
Na Mtume S.A.W anasema: Mtu yoyote atakayemtendea Wema Mtoto Yatima wa kike au wa kiume , basi mimi na yeye Peponi tukakuwa kama vidole hivi, na akaashiria kwa kidole cha Pili na cha kati.
Na anasema Mtume wetu. S.A.W: Nyumba iliyo bora zaidi kwa Waislamu ni nyumba yenye Mtoto Yatima anayetendewa Wema. Na nyumba yenye Shari kuliko zote kwa Waislamu ni ile yenye Yatima anayetendewa uovu.
Na anasema Mtume wetu S.A.W: Mlezi wa Yatima wake au wa mwingine, mimi na yeye tutakuwa pamoja Peponi. Akaashiria kwa kidole chake cha pili na cha kati.

Ewe Mola wetu tunakuomba utujaalie tuwe ni wenye kusikia maneno na wakayafuata yaliyo bora zaidi, wale ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu amewaongoa na hao ndio wenye akili.
Na Dua yetu ya mwisho ni Alhamdulillahi Rabi Alaalameen.